

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI).**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA.**

SIMU:

0713203925 - M/SHULE

S.L.P. 145,

0625736140 - MAKAMU M/SHULE

KYELA.

Email: [ikolosecondary@yahoo.com](mailto:ikolosecondary@yahoo.com)

08/12/2020

**SHULE YA SEKONDARI IKOLO**

Tafadhali unapojibu rejea:

KUMB.Na.IKLSS/JO/VOL.I/17

MWANAFUNZI .....

S/M .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKOLO MWAKA 2021**

- 1.** Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii. Shule ipo katika kata ya IKOLO yapata kilometa saba (07) kutoka Kyela mjini zilipo ofisi za halmashauri au kilometa tatu(03) baada ya kuvuka daraja la mto Kiwira(Ipyana).

Muhula wa masomo kwa mwaka 2021 utanza tarehe 11/1/2021 lakini unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/12/2021

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1. SARE YA SHULE**

**a). WAVULANA**

- i) Suruali 1 rangi ya bluu iliyoiva(deep blue).
- ii) Shati nyeupe mikono mifupi(aina ya tetron)
- iii) Suruali 1 rangi ya khaki
- iv) Shati nyeupe mikono mirefu.

N.B. Suruali iwe na mifuko ya kawaida(isiyo ya jinsi), upana wa chini nchi 16, iwe na marinda mawili, flaizi ya nchi 6 au 7 na urefu unaofunika soksi na usiovuka kisigino.

## **b). WASICHANA**

- i) Sketi 1 ya rangi ya bluu iliyoiva(deep blue).
- ii) Shati nyeupe mikono mifupi(aina ya tetron).
- iii) Sketi 1 ya rangi ya khaki.
- iv) Shati nyeupe mikono mirefu.

N.B. Sketi iwe ndefu inayofunika soksi ,marinda ya kawaida yenye upana wa nchi 3 kila moja na tofauti kati ya rinda moja na jingine ni nchi 2.5, Belt/mkanda wenye upana wa nchi 2 , na upana wa chini usiopungua nchi 110.

## **c). MAHITAJI YA JUMLA.**

- i) Tai ya rangi ya khaki .
- ii) Viatu vyeusi vya kamba(vyenye visigino vifupi) jozi 02.
- iii) Soksi nyeupe jozi 2
- iv) Tracksuit 1 ya rangi ya bluu mpauko (light blue) kwaajili ya michezo
- v) Daftari kubwa (counter book) kumi (10),peni, mkebe wa hisabati(mathematical set) na dictionary (English - English).
- vi) Begi la kuchukulia daftari.

N.B .i) Rambo hairuhusiwi

ii) Viatu vya plastiki haviruhusiwi

## **3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

3.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.Utatakiwa kuzingatia mambo yote ya msingi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

- a) Heshima kwa niongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
- b) Mahudhurio mazuri katia shughuli zote za ndani na nje ya shule ni muhimu
- c) Kuwahi shuleni na katika shughuli zingine utakazopangiwa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuwepo ndani ya eneo la shule wakati wote.
- e) Kutunza usafi wa mwili wako, sare na mazingira ya shule kwa ujumla.
- f) Kuvaa sare ya shule inayotakiwa kwa siku husika.
- g) Kuzingatia ratiba ya masomo na ratiba nyingine za shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za umma.

### **3.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA WEWE KUFUKUZWA SHULE.**

- 1. Wizi.**
- 2. Uasherati, ukabaji, na ushoga.**
- 3. Matumizi ya madawa ya kulevya.**
- 5. Makosa ya jinai.**
- 6. Kupiga aukupigana.**
- 7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
- 8. Kudharau bendera na wimbo wa Taifa.**
- 9. Kuoa au kuolewa.**
- 10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.**
- 11. Kutoa mimba**
- 12. Kuchochea, kushiriki au kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.**
- 13. Kukataa adhabu kwa makusudi**
- 14. Kuwa na simu ya mkononi shuleni au nje ya shule.**

#### **4. MAMBO MENGINE MUHIMU**

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na uongozi wa shule.

5. Tafadhali soma kwa umakini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia maandalizi mema.

**“KARIBU SANA IKOLO SEKONDARI”**

.....

MSUYA, E

MKUU WA SHULE